# Kanuni za Ufundishaji

MWONGOZO 6

## Maendeleo ya Kitaaluma ya Mwalimu: Msaada kwa Walimu Unaoendelea

### UTANGULIZI

Programu ya mafunzo ya walimu ya kanuni za kufundishia (SP) kama ilivyoelezwa katika Mwongozo wa 5, ni muhimu kwa kuanzisha mbinu na njia mpya, kujua nyenzo mpya, na kuziandaa ili kujarib njia hizi mpya. Hata hivyo, mafunzo ya mara moja, au hata matukio ya mfululizo wa mafunzo yaliyotengwa – hayatabadilisha utendaji wa mwalimu kwa kiasi kikubwa.

Baada ya tukio la mafunzo ya walimu, yaliyolenga msaada kwa mwalimu unaoendelea (yaani. ufundishaji wa nje au unasihi elekezi katika skuli, vikundi vya walimu vya kujifunza, msaada wa mbali kupitia teknolojia ya kidijitali) husaidia kuhakikisha kwamba walimu wanatumia nyenzo hizo ipasavyo, na huongeza uaminifu wa utekelezaji. Msaada unaoendelea pia huchangia hamasa ya walimu kutekeleza, kwa kuongeza kujiamini kwao katika kutekeleza ujuzi mpya, kwa sababu ufuatiliaji kutoka kwa mwalimu mkuu au maofisa wa elimu huonyesha uongozi na matarajio ya utekelezaji, na kwa sababu mara nyingi wanajisikia kuunganishwa na kuvutiwa wakati wanapoona mafanikio ya wanafunzi wao.

Mwongozo wa 5, Maendeleo ya Kitaaluma ya Mwalimu: Mafunzo ya Walimu, yanayozingatia matukio ya mafunzo ya walimu ambapo walimu wametambulishwa mbinu, njia au nyenzo mpya. Mwongozo huu unajikita katika kutoa msaada unaoendelea kwa walimu baada ya utambulisho na kuweka hatua za kubuni na utekelezaji wa mtindo wa msaada unaoendelea.

### HATUA YA 1. KUBUNI MTINDO WA MSAADA UNAOENDELEA


#### Jikite katika Mahitaji ya Walimu na msaada unaoendelea

Tambua jinsi walimu wanavyojifunza na kubadilisha utendaji wao. Ujifunzaji huu hupitia mzunguko unaorudiwa wa majaribio na tafakuri (tazama Kielelezo cha 1).[1] Msaada unaoendelea unaweza kusaidia walimu:

- **Jaribu tu**. Himiza walimu kujaribu mbinu mpya (mfano., kutumia mtindo wa kutowa taratibu kama vile "Ninafanya, Tunafanya, Unafanya" ili kusikiliza na kutambua sauti za awali) na hakikisha kwamba wanatumia kulingana na mwongozo wa mafunzo na mwongozo wa walimu.
- **Endelea baada ya jaribio la kwanza.** Wasaidie walimu kutatua changamoto wanazokutana nazo wakati wakijaribu maarifa hayo katika muktadha wao (mfano., ni vigumu kufanya na darasa hili kubwa kuliko nilivyojua. Je, ninaweza kufanya nini?).
- **Tazama jinsi inavyofanya kazi**. Saidia na ongoza walimu kutafakari kinachotokea wakati wanapotumia maarifa hayo (watoto wana shauku, watoto wanakuwa bora katika kusikia sauti ya awali, nk.).
- **Amua kitu gani kinafuata.** Wakati walimu wanaimarika au kupata ustadi wa mbinu fulani, wasaidie kuamua wajikite katika kitu gani kinachofuata kwa ajili ya maboresho (mfano., sauti za awali kwa sasa zinaendelea vizuri, lakini kuchanganya na kutenganisha bado ni ngumu).

***Walimu watakapoona maarifa mapya yanafanya kazi, wataendelea kuyatumia. Msaada wa mwalimu unaoendelea unalenga lengo hilo la msingi.***

**KIELELEZO CHA 1.** Mzunguko wa ujifunzaji wa walimu



## Zingatia Mitindo Inayowezekana

Kwa kuzingatia aina ya msaada unaohitajika, kama ilivyoelezwa hapo juu, zingatia mitindo kwa kutolea. Mitindo iliyomaarufu hujumuisha:

- **Unasihi elekezi**. Hii inaweza kuwa unasihi elekezi ndani ya skuli ambapo (mwalimu mkuu, mwalimu mzoefu n.k.) huwaangalia walimu katika ufundishaji na kufanya majadiliano nao baada ya uangalizi. Au unasihi elekezi nje ya skuli, ambapo mnasihi elekezi kutoka nje ya skuli (msimamizi wa mbinu za kufundishia kwa klasta au mfano huo) huzisaidia skuli nyingi, hutembelea skuli na kuchunguza pamoja na kufanya majadiliano na walimu na walimu wakuu kutafakari juu ya ufundishaji wao.
- **Vikundi vya walimu vya kujifunza (CoP)**. Walimu hukutana na kujadiliana kuhusu ufundishaji wao, changamoto wanazokabiliana nazo na kutafakari kwa pamoja. Mikutano inaweza kufanyika miongoni mwa walimu katika skuli au kuwahusisha walimu kutoka katika klasta ya skuli.
- **Msaada wa mbali kwa kutumia teknolojia ya kidijitali**. Usaidizi wa namna mbalimbali unaweza kutolewa katika maeneo ya mbali kupitia njia za teknolojia. Kwa mfano: programu za redio ambazo huwasilisha videkezo vya walimu, video ambazo walimu wanaweza kuangalia wenyewe, simu, ujumbe wa maandishi, rogram mbali mbali za mitandaoni kama vileskype au Whatsapp

Programu nyingi hutumia muunganiko wa mitindo, na kuna ushahidi wa utafiti kwamba kuunganisha njia nyingi inaweza kuwa na ufanisi zaidi.[2] Hata hivyo, ufanisi wa mtindo wowote, au muunganiko wowote, utategemea muktadha na ubora wa utekelezaji.

Kuna ushahidi madhubuti wa umuhimu wa unasihi elekezi ( ); utafiti madhubuti wa kitakwimu umeonyesha athari kwenye matokeo ya ujifunzaji wa wanafunzi pale ambapo unasihi elekezi () unatumika.[3]

Katika Utafiti wa Kusoma Darasa la Awali nchini Afrika Kusini, Cilliers et al. (2018) waligundua kwamba wanafunzi waliokamilisha miaka miwili ya programu hiyo waliimarisha umahiri wa usomaji wao kwa kiwango cha muachano sanifu cha 0.12 iwapo walimu wao walipokea mafunzo ya wote pekee, ukilinganisha na kiwango cha muachano sanifu cha 0.24 iwapo walimu wao walipata mafunzo ya unasihi elekezi ya darasani.

Tafiti chache za kitaalamu zimechunguza vikundi vya walimu vya kujifunza na athari yake kwenye matokeo ya ujifunzaji, kwahiyo kwa sasa kuna ushahidi mdogo wa kuzitegemea kama njia ya awali ya msaada. Hata hivyo, tafiti za ubora zimeonyesha kwamba vikundi vya walimu vya kujifunza ni fursa za muhimu kwa walimu kutafakari na kutafuta njia za kutatua changamoto,[4] zikionyesha kwamba vikundi vya walimu vya kujifunza vinaweza kuwa na umuhimu kama sehemu moja ya mtindo wa msaada. Kama ilivyoelezwa na mwalimu katika programu ya Tusome Shughuli ya Usomaji wa Darasa la Awali nchini Kenya (the Tusome Early Grade Reading Activity), vikao vya vikundi vya walimu vya kujifunza viliwawezesha "kujadili changamoto zinazowakumba walimu hao darasani, kwa hivyo unapokuja darasani, unaimarisha mbinu za kufundishia."

Muunganiko wowote wa mitindo unaochagua, **ni muhimu kuhakikisha kwamba walimu wanaweza kutazamwa na kupewa maoni yanayojenga, na kwamba walimu wana fursa ya kutafakari uzoefu wao wa utendaji mapya**.

Katika utafiti wa ubora wa mikutano ya walimu kwa klasta ya skuli nchini Afrika Kusini, Jita na Mokhele (2014) walibaini kwamba mikutano hii ya tafakuri ilionekana kuongeza maarifa ya maudhui ya walimu na maarifa ya ufundishaji. Mikutano ya klasta pia ilitoa "faida za mchakato" ambazo zilijumuisha ushirikiano, mwongozo wa ufundishaji, na uongozi wa walimu.

**JEDWALI LA 1. Mitindo ya Msaada wa Mwalimu: Faida na Hasara**

| Mtindo | Faida | Hasara |
|---|---|---|
| **unasihi elekezi katika skuli** | Gharama nafuu. Inaruhusu uangalizi/mrejesho wa mara kwa mara. Inaweza kusaidia kuhakikisha kujituma kwa ngazi ya skuli. | Wasimamizi wa skuli mara nyingi wana majukumu mengi kushughulikia jukumu hili. Ni vigumu kufuatilia. Inaweza kuhusisha mafunzo na msaada wa ziada kwa wafanyakazi wa skuli kuchukua jukumu. |
| **Unasihi elekezi wa nje** | Washaurui elekezi ) wanaweza kuwa na mafunzo ya ngazi ya juu na inaweza kuwa njia ya wataalamu wengine kutoa taarifa ya ziada. | Gharama. Iwapo uwiano wa mshauri elekezi (coach) kwa skulini wa mkubwa, au iwapo safari ni ngumu kati ya skuli, walimu wanaweza kupokea ziara chache. |
| **Vikundi vya walimu vya kujifunza ngazi ya skuli** | Mbinu isiyo ya gharama. Inaweza kuunda mazingira chanya ya skuli kwa kujaribu mbinu mpya. | Ina ufanisi mdogo ikiwa walimu ni wachache kwa skuli. Bila msaada wa kutosha, vikao pia vinaweza kupoteza mwelekeo au kuimarisha mitazamo isiyo sahihi. |
| **Vikundi vya walimu vya kujifunza ngazi ya klasta** | Inaweza kuwa gharama nafuu na kuweza kuwapa nguvu walimu. Inaweza kuwa na ufanisi kwa kutafuta utatuzi wa matatizo au masuala. | Vikundi vinahitaji mud na bajeti kwa ajili ya walimu kukutana. Pia, vinahitaji msaada na mchango wa kiufundi kuhakikisha kwamba utafutaji wa suluhu wa pamoja unafaa kiufundi. |
| **Saidia kupitia teknolojia ya kidijitali** | Inaweza kusaidia kuondoa mapengo ambapo mawasiliano ya ana kwa ana ya mara kwa mara hayawezekani, au ambapo mtaalamu hawezi kutembelea skuli zote mara kwa mara. | Inakuwa na ufanisi zaidi pamoja na mbinu nyingine. Mtandao na ufikiaji wa vifaa vya kidijitali lazima kuzingatiwa. |

## Zingatia Muktadha

Chunguza muktadha ili kutambua yafuatayo.

- Rasilimali zilizopo. Taratibu kwa ajili ya msaada wa mwalimu tayari zipo, au baadhi zilikuwepo siku za nyuma? Mifano inaweza kuwa chaguzi za mfumo wa serikali, au taratibu zilizotekelezwa na mashirika yasiyo ya kiserikali. Iwapo jibu ni ndiyo, jifunze kile ambacho kimefanya kazi au ambacho hakijafanya kazi, na ujenge juu ya maarifa hayo.
- Mazingatio ya taratibu. Je, ni sifa zipi zinazoziua (au zinazowezesha) za jiografia, demografia na utumishi? Kwa mfano: Je, skuli zipo karibu, kwamba mwalimu anaweza kusafiri kwa urahisi miongoni mwa skuli hizo, au inachukua siku kadhaa kusafiri? Je, mwalimu mkuu pia ana jukumu kamili la kufundisha? Je, mfumo wa elimu uliopo una nafasi za msaada kwenye kanuni za kufundishia na zimetengewa bajeti kikamilifu? Je, intaneti au mtandao wa simu unaruhusu kutowa msaada kupitia teknolojia ya kidijitali?

Katika nchi nyingi, majibu ya maswali haya yatatofautiana kulingana naeneo, kwa hivyo unaweza kuhitaji mtindo unaoweza kubadilika. Kwa mfano, katika eneo la Terai (uwanda wa chini) la Nepal, skuli zipo nyingi na zinakaribiana, kwa hivyo unasihi elekezi wa nje ufundishaji wa nje na vikundi vya walimu vya kujifunza ngazi ya klasta vinaweza kuwa na maana. Katika maeneo ya mlima Himalaya, kwa upande mwingine, skuli ziko mbali kutoka moja hadi nyingine na ni vigumu kusafiri kuzifikia kwa sababu ya miinuko na hali ya hewa. Katika hali hizo, kuunganisha unasihi elekezi katika skuli pamoja na ziara za msaada wa nje wa mara kwa mara na mawasiliano yasiyo ya ana kwa ana yanaweza kufaa zaidi.

## HATUA YA 2. MIPANGO YA UENDESHAJI

Mara moja utakapokuwa na wazo la mitindo unayowezekana na uielewa wa muktadha, unaweza kugeukia kuanza kupanga taarifa za uendeshaji ili kujaza katika muundo. Unapofanya hili, weka uendelevu—yaani uwezo wa kuendelea programu ya SP kwa muda mrefu, pamoja na rasilimali za serikali tu—mbele na katikati.

### Utafiti wa Uendeshaji na Ufuatiliaji

Kuelewa kilichofanya kazi siku za nyuma ni sehemu nzuri ya kuanzia. Ufuatiliaji wakati wa kuanza kwa mtindo mpya wa msaada wa walimu utakusaidia kupata mahali ambapo utekelezaji unahitaji kuimarishwa. Kwa mfano, iwapo data za ufuatiliaji zinaonyesha kwamba wakufunzi hawazingatii mafunzo mara kwa mara, ndipo unaweza kutambua vikwazo na kuvitatua ili uchunguzi uendelee. Utafiti wa uendeshaji unaweza kukusaidia kutambua njia ambazo unaweza kuhitaji ili kurekebisha mtindo ili kuhakikisha uendelevu.

### Mazingatio ya Bajeti

Kuwa mkweli kuhusu bajeti lakini pia iwe inafaa kiufundi. Programu nyingi zilizowezeshwa kwa fedha za ndani zina msaada mkubwa uliojengwa ndani yake. Hata kama zinaonyesha matokeo mazuri, hata hivyo, chaguzi hizo zinaweza kuwa za gharama sana kwa serikali kuzichukua baadaye. Kwa maneno mengine, mitindo hii ya msaada inaweza kuwa inafaa kiufundi lakini haina uhalisia kwa bajeti. Kinyume chake, mifumo ya serikali mara nyingi hupunguza bajeti kwa ajili ya msaada wa walimu katika kiwango cha kutokuwa na ufanisi. Chaguzi hizi zinaweza kuwa na uhalisia wa bajeti lakini zisiwe zinafaa kiufundi.

Unaweza kufanya kazi na serikali ili kutambua mbinu za gharama nafuu – kama vile mbinu zenye ufanisi kwa malipo ya safari – ambazo bado zinaruhusu msaada wa kutosha kwa walimu. Wakati wa mchakato huu, pia jaribu kuweka uwiano mipango ya uendelevu pamoja na kuingiza fedha kwa kuanzia na uthibitisho wa dhana. Programu inapoanza, jaribu kuwa na mazungumzo endelevu na serikali kutetea kwa ajili ya kulinda bajeti ya kutosha kwa msaada wa walimu. Kufanya kazi kwa karibu na serikali juu ya mtindo wa msaada wa walimu na kufanya waone matokeo chanya kutachangia katika majadiliano hayo.

UTAFITI WA UENDESHAJI UNAWEZA KUKUSAIDIA KUTAMBUA NJIA AMBAZO UNAWEZA KUHITAJI KUREKEBISHA MTINDO HUO ILI KUHAKIKISHA UENDELEVU

### Rasilimali Watu

Kwa kadri inavyowezekana, mtindo wa msaada wa mwalimu unapaswa kutumia nafasi za serikali zilizopo. Programu za nje zinapoajiri wanasihi elekezi moja kwa moja, nafasi hizo za unasihi elekezi, na wataalamu ambao wanazijaza, mara chache huhamishia katika mfumo wa serikali. **Wakati huo huo, mifumo mingi ya serikali ina nafasi ambazo mwanzoni ilikusudiwa kutoa msaada wa kanuni za kufundishia lakini imekuwa ya kiutawala na kuzidiwa na majukumu mengine**.

Ili kufikiria upya nafasi hizi kwa kutoa msaada wa walimu, shauriana na serikali ili kuwahimiza kurekebisha au kuunda maelekezo mapya ya kazi (tazama Mwongozo wa 1 kuhusu usimamizi wa serikali na utumiaji wa walimu). Au iwapo mfumo una wanasihi elekezi, tathmini ikiwa itawezekana kupunguza idadi ya skuli ambazo mnasihi elekezi anawajibika nazo. Mwisho, wakati mwingine wafanyakazi katika nafasi hizo hujiona na kama wanavyoonwa na wafanyakazi wa skuli, kama "wakaguzi" kuliko kama wanasihi elekezi au washauri wa kitaaluma. Iwapo ndivyo ilivyo, watahitaji mafunzo na msaada thabiti ili kuhamisha mwelekeo wao.

## Uwajibikaji na Motisha

Kama ilivyojadiliwa katika [Mwongozo wa 7](#) kuhusu data, mifumo, na uwajibikaji, utahitaji kufanya kazi na serikali ili kuhakikisha kwamba mfumo wa msaada wa mwalimu umeungana na taratibu za uwajibikaji. Katika njia hiyo, unaweza kufuatilia unasihi elekezi ( ) na vikundi vya walimu vya kujifunza, ngazi za uwajibikaji ziko wazi, na unaweza kutoa msaada uliolengwa iwapo utekelezaji umekwama. Hakikisha motisha za watendaji katika mfumo wa msaada zipo, kwa kuwa wanafanya kazi ngumu ya kubadilisha ufundishaji. Hii inaweza kujumuisha, kwa mfano, daraja ya mafunzo, kupandishwa ngazi au kutambuliwa kuwa mnasihi elekezi au mwezeshaji wa vikundi vya wealimu vya kujifunza, na tuzo au barua ya kutambuliwa.

## HATUA YA 3. KUJAZA TAARIFA ZA KIUFUNDI

Mara muundo wa msingi wa msaada wa mwalimu unapotafsiriwa, unaweza kujaza taarifa. Sehemu hii imejikita katika unasihi elekezi/ushauri wa kitaaluma, vikundi vya walimu vya kujifunza, na kuingiza teknolojia ya kidijitali. Maelekezo mengi yanayopendekezwa hapa yalianzia katika utafiti wa mwaka 2018 ambao RTI International ilifanya kuhusu msaada wa walimu unaoendelea katika programu kubwa za SP duniani kote, ambao ulipelekea miongozo ya kutekeleza unasihi elekezi na vikundi vya walimu vya kujifunza.[5]

### Unasihi elekezi/ushauri wa kitaaluma

- **Fundisha na saidia wanasihi elekezi**. Wanasihi elekezi wanahitaji mafunzo na msaada wa njia za kuelekeza na ujuzi wa kufundisha. Fundisha wanasihi elekezi kukuza uhusiano na walimu ambao unalenga kushauri, kuliko tathmini au ukaguzi. Waongoze kutowambia walimu wafanye nini, lakini badala yake kusikiliza na kuwaacha walimu wafikirie kuhusu mazoezi yao wenyewe. Hili linahitaji kuwa lengo la mara kwa mara la kufundisha na kusaidia wanasihi elekezi.
- **Tumia zana za uangalizi ambazo ni fupi, rahisi na zinazingatia vipengele muhimu vya kufundisha**. Sanifu zana ili kujikita katika sehemu ambazo ni muhimu zaidi kwa masomo na kulenga Mazoezi muhimu ya ufundishaji. Unda zana hizi rahisi, za moja kwa moja na rahisi kwa wanasihi elekezikutumia na zilizojikita katika msaada wa kujenga kuliko kuwa za ukaguzi au tathmini.
- **Weka kipaumbela tabia ya ufundishaji katika awamu**. Anza na ujuzi ambao utakuwa rahisi kwa walimu kujifunza na kwenda kwenye mgumu zaidi baada ya muda – kama vile kuanza na taratibu za kutambulisha herufi, hatimaye kujenga jinsi ya kuunda maswali mazuri ya uelewa (kulingana na mzunguko wa kujifunza wa mwalimu, Kielelezo cha 1). Inapowezekana, zingatia maeneo ya kuimarisha ambayo walimu wao wenyewe wameonyesha.
- **Hakikisha kwamba vikao vya mijadala vya wanasihi elekezibaada ya uchunguzi vinajumuisha tafakuri na mijadala ya walimu kuhusu kipi kilifanikiwa vema na kipi cha kuelekeza uangalizi zaidi**. Wanasihi elekeziwanapaswa kuwapa walimu nafasi kwanza ili kutafakari kuhusu somo lao. Kisha, wanasihi elekeziwanapaswa kutoa mrejesho chanya. Mwisho, wanasihi elekezi, pamoja na walimu, waainishe maeneo mawili au matatu ya kuimarisha ambayo yako wazi, mahsusi, na yanayotekelezeka.
- **Zingatia kujumuisha tathmini fupi za wanafunzi wakati wa ziara za unasihi elekezi**. Panga kwa ajili ya wanasihi elekezikupima sampuli ndogo ya wanafunzi baada ya kila ziara ya uchunguzi wa darasa, kwa jumla isichukue zaidi ya dakika tano, kama vile kuchagua wanafunzi watatu wa darasa la kwanza na kuwataka wasome maneno Matano yasiyopangiliwa kutoka kwenye somo. Maingiliano haya yatawapa wanasihi elekeziwazo la maendeleo ya wanafunzi, ambalo wanatumia kusaidia walimu kufanya maamuzi ya ufundishaji.

### Vikundi vya walimu vya kujifunza

- **Toa mafunzo na msaada kwa uwezeshaji wa vikundi vya walimu vya kujifunza** . Fundisha viongozi au wawezeshaji wa Vikundi vya walimu vya kujifunza kuhusu utendaji halisi ulio muhimu katika ufundishaji pamoja na kupanga ajenda za Vikundi vya walimu vya kujifunza, na kuongoza vipindi Vya Vikundi vya walimu vya kujifunza vyenye ufanisi. **Ni rahisi kwa vikao vya Vikundi vya walimu vya kujifunza kupoteza mwelekeo, kuruhusu taratibu na utawala kukiuka ufundishaji, au kuchanganyika pamoja na vikao vya wafanyakazi**. Usimamiaji na ufuatiliaji unahitajika ili kusaidia kuepuka hili, au kuelekeza tena viongozi na vikao hivyo iwapo vurugu zinaanza kutokea.
- **Hakikisha vikao vya klasta viko vimetengenezwa vizuri**. Mwongozo uliotolewa kwa Vikundi vya walimu vya kujifunza unapaswa kutoa muundo unaotosha ili kuwezesha vikao vinavyojenga, wakati ukiruhusu ubadilikaji na chaguo la washiriki. Mfumo wa ajenda unaweza kujumuisha mifano ya shughuli, pamoja na mapendekezo ya mada. Shughuli lazima zijumuishe:
    - Ongoza mazungumzo ya tafakuri na majadiliano (ukiwa na sampuli ya maswali ya tafakuri)

"NILIKUWA NIMEJIFUNZA UJUZI KATIKA MAFUNZO, LAKINI NI UNASIHI ELEKEZIAMBAO ULINIFANYA NIJIAMINI KATIKA KUTUMIA UJUZI HUO. NILIPOTEA MARA YA KWANZA LAKINI MNASIHI ELEKEZI ALINIONGOZA." - MWALIMU NCHINI NEPAL AKIJADILI MFUMO WA MSAADA WA WALIMU WA NEGRP

- Ainisha changamoto za kawaida na bungua bongo kupata suluhisho – kama vile jinsi ya kupima wanafunzi katika darasa kubwa, au jinsi ya kuhakikisha wanafunzi wote wanashiriki
- Onesha ufundishaji wa somo, na utoe mrejesho
- Tazama na jadili mtindo kwenye video zilizorekodiwa za mwalimu

- Toa ufikiaji wa msaada wa ziada wa kiufundi iwapo//kama inavyohitajika. Walimu wanapata mengi kutokana na kubadilishana uzoefu miongoni mwao wenyewe, lakini pia wanahitaji kupata mtu mwenye utaalamu zaidi katika mazoezi ya ufundishaji yaliyolengwa, ambaye wanaweza kumuomba msaada. Mshauri huyu pia anaweza kuhakikisha kwamba suluhisho zilizoundwa na walimu zinafaa kiufundi. Mtu huyu anaweza asiahudhurie vikao vya Vikundi vya walimu vya kujifunza lakini atakuwa nyenzo ya kuiomba kadri inavyohitajika, au kuwasiliana na Vikundi vya walimu vya kujifunza mara kwa mara. Iwapo muundo wa programu yako utajumuisha Vikundi vya walimu vya kujifunza pamoja na unasihi elekezi, mnasihi elekezi/mshauri wa kitaaluma anaweza kuhudumu katika nafasi hii.

**Mbinu Zinazotumainisha za Teknolojia ya Kidijitali**

**Teknolojia ya kidijitali inaweza kutoa njia za gharama nafuu ili kuongeza msaada. Baadhi ya mifano inayotumainisha ni:**

- Wanasihi elekeziwanatumia **SMS** (ujumbe mfupi wa maandishi) kutuma kikumbushi na dondoo na kujibu maswali ya mwalimu.
- Walimu wanafanya mazungumzo ya Vikundi vya walimu vya kujifunza kwa njia isiyo ya ana kwa ana, kupitia **majukwaa kama vile WhatsApp, Viber, au Skype**.
- Walimu wanapata moduli za kujifunzia na dashibodi za mwingiliano, kulingana na mahitaji na kuvutiwa kwao, kupitia**majibu ya mwingiliano wa sauti** na **majukwaa ya elimu ya mtandaoni**.

## HITIMISHO

Je, walimu watajaribu na kisha kuendelea kutumia mazoezi yao ya ufundishaji ambayo yameunganishwa kwenye nyenzo na kutambulishwa wakati wa mafunzo? Jibu la swali hili lipo katikati ya utekelezaji. Iwapo walimu wengi hawajaribu kutumia nyenzo za kanuzi za kufundishia, au wamekata tamaa baada ya jaribio moja au mawili ya mbinu mpya kutoka kwenye mafunzo, programu hiyo haitakuwa na athari zilizokusudiwa kwa kusomo, kuandika na kuhesabu kwa wanafunzi.

Msaada wa walimu unaoendelea utasaidia kuhakikisha kwamba sehemu hii muhimu ya fumbo la mbinu za kufundishia zilizoratibiwa inaangukia mahali pake. Ingawa hakuna fomula moja ya ajabu ya msaada wa walimu ambayo itafanya kazi kila sehemu, kama ambavyo mwongozo huu umejadili, unaweza kujifunza vya kutosha kutoka kwenye uzoefu na tafiti ili kufanya maamuzi mazuri kuhusu kile kinachoweza na kinachofaa kiufundi katika muktadha fulani. Kisha panga kuwasilisha ufuatiliaji na utafiti wa uendeshaji ili kuthibitisha kwamba walimu wanapokea msaada unaoendelea wanaohitaji ili wafanikiwe, na kufanya programu ya SP iwe na athari.

Kuhusu alama katika mwongozo huu:

Huonyesha "Tahadhari Nyekundu": Kitu cha kukijua na kuchukua tahadhari, kwa sababu ni tatizo la kawaida

Huonyesah "Isiyojadiliwa": lazima kuwa nayo

## RASILIMALI

Craig, Kraft na du Plessis wanatoa muhtasari, kwa mifano, wa mazoezi bora katika mafunzo na msaada wa walimu: https://people.umass.edu/educ870/teacher_education/Documents/Craig-book.pdf

Nyenzo ya Mtandao wa Kimataifa wa Usomaji inatoa mapendekezo na kujadili mifano ya programu thabiti za ufundishaji: https://pdf.usaid.gov/pdf_docs/PA00TXZ9.pdf

Juzuu, imehaririwa na Pouezevara, wa utafiti kisaunaohusu aina mbalimbali za mitindo ya msaada unaoendelea: https://www.rti.org/rti-press-publication/cultivating-dynamic-educators

Piper, Mejia, na Betts wanawasilisha kuhusu utafiti wa nchi nzima juu ya unasihi elekezi na Vikundi vya walimu vya kujifunza. ***Yaliyoruhusiwa na Yasiyoruhusiwa kuhusu uimarishaji wa Ufundishaji Kupitia Msaada wa ufundishaji: Matokeo kutoka Utafiti wa Nchi Nyingi wa unasihi elekezi na Vikundi vya walimu vya kujifunza i***. Andiko liliandaliwa kwa ajili ya mkutano wa mwaka wa Jumuiya ya Elimu Linganishi na ya Kimataifa.

Funda Wande: kufundisha video ambazo zinaweza kutumika wakati wa mikutano ya Vikundi vya walimu vya kujifunza kwa ajili ya majadiliano, pamoja na video ambavyo walimu wanajadiliana mazoezi yao: https://fundawande.org/video-resources

Video kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), ikielezea matumizi yenye ufanisi ya unasihi elekezi uliounganishwa wa ana kwa ana na usio wa ana kwa ana katika Ulimwengu wa Tatu, na kuonyesha baadhi ya unasihi elekezi huu kwa vitendo. https://www.usaid.gov/news-information/videos/coaching-teachers-south-africa-produces-results

Complete Series of Structured Pedagogy How-To Guides: https://scienceofteaching.site/how-to-guides/

## UTAALAMU WA KIUFUNDI UNAHITAJIKA

Wataalamu katika mazoezi ya ufundishaji yaliyolengwa na katika msaada wa kitaaluma wa mwalimu – kwa hatua ya kubuni na kisha kwa ajili ya kuendeleza zana na mafunzo.

**REJEAO**

1 Mtindo huo katika Kielelezo cha 1 ni kulingana na mitindo iliyowasilishwa: Guskey, Thomas R. 1986. "Staff Development and the Process of Teacher Change." *Mtafiti wa Elimu* 15, no. 5: 5–12; Kolb, David. 1984. *Kujifunza kwa Uzoefu: Uzoefu kama chanzo cha Elim na Maendeleo*. Upper Saddle River, NJ: Prentice Hall; na Smith, Margaret Schwan. 2001. *Maendeleo ya Kitaaluma kwa Vitendo kwa Walimu wa Hisabati*. Reston, VA: Baraza la Taifa la Walimu wa Hisabati.

2 Tazama, kwa mfano: Craig, Helen J., Richard J. Kraft, and Joy du Plessis. 1998. *Teacher Development: Making an impact*. Produced for USAID under the Advancing Basic Education and Literacy Project; and for the World Bank by the Human Development Network, Effective Schools and Teachers. Washington, DC: Academy for Educational Development (AED) and World Bank. https://people.umass.edu/educ870/teacher_education/Documents/Craig-book.pdf; Darling-Hammond, Linda E., Maria E. Hyler, and Madelyn Gardner. 2017. *Effective Teacher Professional Development*. Palo Alto, CA: Learning Policy Institute. https://learningpolicyinstitute.org/sites/default/files/product-files/Effective_Teacher_Professional_Development_REPORT.pdf; Westbrook, Jo, Naureen Durrani, Rhona Brown, David Orr, John Pryor, Janet Boddy, and Francesca Salvi. 2013. *Pedagogy, Curriculum, Teaching Practices and Teacher Education in Developing Countries*. Final Report. Education Rigorous Literature Review. Prepared by the Centre for International Education, University of Sussex. London: UK Department for International Development. https://assets.publishing.service.gov.uk/media/57a08a13ed915d622c00054f/Pedagogy-curriculum-teaching-practices-education.pdf

3 Mifano ya tafiti hizo inajumuisha: Cilliers, Jacobus, Brahm Fleisch, Cas Prinsloo, and Stephen Taylor. 2018. *How to Improve Teaching Practice? Experimental Comparison of Centralized Training and In-Classroom Coaching*. RISE Working Paper. https://riseprogramme.org/sites/default/files/publications/RISE_WP-024_Cilliers_TeachingPractice.pdf; Piper, Benjamin, Stephanie Simmons Zuilkowski, Margaret M. Dubeck, Evelyn Jepkemei, and Simon J. King. 2018. "Identifying the Essential Ingredients to Literacy and Numeracy Improvement: Teacher Professional Development and Coaching, Student Textbooks, and Structured Teachers' Guides." World Development 106, June: 324–336. https://doi.org/10.1016/j.worlddev.2018.01.018.

4 Kwa mifano tazama: Pouezevara, Sarah R., ed. 2018. *Cultivating Dynamic Educators: Case Studies in Teacher Behavior Change in Africa and Asia*. RTI Press Publication No. BK-0022-1809. Research Triangle Park, NC: RTI Press; Jita, Loyiso C., and Matseliso L. Mokhele. 2014. "When Teacher Clusters Work: Selected Experiences of South African Teachers with the Cluster Approach to Professional Development." South African Journal of Education 34, no. 2: 1–15. https://doi.org/10.15700/201412071132; Foundation for Educational Change (FEDUC). 2020. *Study on Effectiveness of Teacher Professional Support System in Early Grades*. Final Report. Prepared for USAID under the Early Grade Reading Program in Nepal, Contract No. AID-367-TO-15-00002. Research Triangle Park, NC: RTI International.

5 Piper, Benjamin L., Jessica Mejia, and Kellie Betts. 2020. *Do's and Don'ts of Improving Teaching Through Instructional Support: Findings from a Multi-Country Study of Coaching and Communities of Practice*. Paper prepared for the annual meeting of the Comparative and International Education Society.

Hati hii imepewa leseni chini ya Creative Commons Attribution 4.0 Leseni ya Kimataifa. .

Mwongozo umeandikwa na **Dkt. Wendi Ralaingita**